# MISINGI YENYENGUVU

**MMOJA-KWA-MMOJA**

Dynamic Churches
International

***Dynamic Churches International***
Simeon Oyui
P. O. Box 798-00515
Bukubura, Nairobi, Kenya
EAST AFRICA
Email: ncc_africa@yahoo.com

***Dynamic Churches International***
164 Stonegate Close
Airdrie, Alberta T4B 2V2
Canada.
E-Mail dcioffice@shaw.ca



Vifungu vya Biblia vilivyonakiliwa katika kitabu hiki vyote ni kutoka kwa Biblia Habari Njema toleo la 1995, na ile ya muungano wa mashirika 1994, 1952, 1989.



© 2016 Dynamic Churches International.
Haki zote zimehifadhiwa.

# MISINGI YENYE NGUVU

## MMOJA-KWA-MMOJA
## WALIOKUSUDIWA

Ukufunzi wa Mmoja-kwa-Mmoja umekusudiwa kwa manufaa ya wale wote waliokwisha kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao kibinafsi, huku wakijitoa muhanga kukua katika uhusiano wao mpya na Mungu. Hivyo sote kwa pamoja tunajitoa kwa Mungu.

## SHUKURANI

Mafunzo haya yametayarishwa kwa njia nzuri zaidi ili yaweze kumsaidia Mkristo mchanga kukua katika imani na mwenendo wake na Mungu, na aweze kuwashirikisha wengine. Shukurani kwa wale wote waliochagua maandalizi haya.

***" Basi, yeyote akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, na yote yamekuwa mapya!"***

2 Wakorintho 5:17

*Dynamic Churches International*

**Al Middleton – Executive Director**
164 Stonegate Close
Airdrie, AB T4B 2V2, CANADA
Email: dcioffice@shaw.ca

**Simeon Oyugi - Kenya Rep.**
P O Box 798-00515
Buruburu, Nairobi, Kenya E Africa
ncc_africa@yahoo.com

Vifungu vyote vya maandiko vilivyonakikiliwa katika chapa hii ni kutoka kwa Biblia Habari Njema toleo la 1995, na ile ya Muungano wa Kimataifa wa Mashirika ya Biblia 1994, 1952, 1989.

Copyright © 2016 Dynamic Churches International.
Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| | **Ukurasa** |
| 1. MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO | 1 |
| 2. MAISHA MAPYA KATIKA USHINDI | 5 |
| 3. MAISHA MAPYA YENYE UWEZA | 9 |
| 4. MAISHA MAPYA YENYE USAWA | 13 |
| 5. UKUFUNZI WENYE NGUVU - NAFASI NZURI | 17 |
| 6. MISINGI YENYE NGUVU<br>TARATIBU YA VIONGOZI | 19 |
| 7. CHETI CHA KUHITIMU | Ukurasa wa Nyuma |

# MISINGI YENYE NGUVU

Somo la Kwanza

**MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO**

Kumpokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako binafsi ndio mwanzo wa uhusiano wa milele, inakupa uwezo wa ajabu wa maisha ya furaha hapa duniani na hata mbinguni.

Katika kipindi hiki tutajifunza:
1. Maisha ya uzima wa milele.
2. Manufaa ya kumjua Yesu Kristo kibinafsi.
3. Jinsi unavyoweza kuwa na hakika ya kwamba wewe ni wa Yesu Kristo.

**1. UZIMA WA MILELE NI KUMJUA MUNGU KIBINAFSI**

> ***" Na uhai wa milele ndio huu: kukujua wewe uliye peke yako Mungu wa kweli, na kumjua Yesu Kristo uliyemtuma."***
>
> Yohana 17:3

"Uzima wa Milele" ni zaidi ya maisha marefu; ni maisha mapya kamili - aina ya maisha aliyo nayo Mungu, yasiyo na vikwazo vyovyote. Upendo wa Mungu haubagui dhamani wala hali ya kupendeza watu. Yohana 3:16 yasema, ***"Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uhai wa milele."*** Kadhalika Mungu hana mpaka wa uvumilivu, wema, msamaha ama kwa njia yoyote.

Kuwa na "Uzima wa Milele" ni kwamba unayo nafasi ya kuishi maisha tele yenye maana.

Kuna faida gani unapoingia kwenye utimilifu wa maisha mapya?

## 2. FAIDA ZA KUMJUA YESU KRISTO KIBINAFSI

Soma kila kifungu kisha ulinganishe na mawazo yafananayo. (Unganisha alama ndogo)

| FUNGU | YALE MUNGU ALIYONIFANYIA | FAIDA NINAYOPATA |
|---|---|---|
| Warumi 5:8 | Mungu alinidhihirishia Upendo wake • | • Mambo ya kale yamepita na tazama yamekuwa mapya |
| Wakolosai 1:13,14 | Mungu alinikomboa kutoka kwa ufalme wa giza• | • naweza kutosheka |
| 2 Wakorintho 5:17 | Mimi ni kiumbe kipya • | • nikiwa mwenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yangu |
| Ufunuo 3:20 | Kristo aliingia maishani mwangu • | • Sitaangamia kamwe |
| Waebrania 13:5 | Kristo hataondoka • | • Aliniingiza katika ufalme wa mwanawe |
| Yohana 10:28 | Yesu alinipa uzima wa Milele • | • Alinileta kwa Mungu |
| 1 Petro 3:18 | Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zangu • | • Naweza kuwa na ushirika naye |

Faida hizi zote ni kwa ajili ya upendo wa Mungu, nazo hupatikana tunapomtumaini yeye kwa yote aliyofanya.

Tazama Waefeso 2:8, 9 kisha ujalize sehemu tupu.

***"Kwa maana mmekombolewa kwa __________, kwa njia ya _________; ambayo hiyo haikutokana na _______________, ni _______________ cha _________________; wala sio kwa ______________, mtu awaye yote asije akajisifu."***

Wokovu unawezekana tunapoweka imani yetu katika:
(Piga msitari chini ya jawabu sahihi)

1. Yale unayoweza kufanya
2. Yale ambayo Yesu Kristo amefanya
3. Yale ambayo kanisa lako limefanya
4. Yale ambayo wazazi wako wamefanya

## 3. UHAKIKA WA KUWA NDANI YA YESU KRISTO

Soma Yohana 3:16
Mungu alikuwa na lengo gani? ____________________________________

Mungu alifanya nini? ____________________________________________

Ni nani angefaidika? ____________________________________________

Wangepata nini? _______________________________________________

Soma Ufunuo wa Yohana 3:20
Njia moja ya kuonyesha imani katika Kristo ni ________________________

_____________________________________________________________

Jukumu lako ni nini? ____________________________________________

Jukumu la Mungu ni nini? ________________________________________

Je, umemkaribisha Kristo katika maisha yako? Yuko wapi sasa?

_____________________________________________________________

Kama huna uhakika na wokovu wako, waweza kuwa na uhakika unapompokea Kristo sasa hivi kwa kuamua na kumkubali yeye.

Omba ombi hili:

> **Bwana Yesu, mimi ni mwenye dhambi na siwezi kujiokoa mwenyewe. Asante kwa kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu. Karibu maishani mwangu ili uwe mwokozi na Bwana wangu. Asante kwa kunisamehe dhambi zangu na kunipa uzima wa milele. Chukua uongozi wa maisha yangu na uzima wako wa milele ukae ndani yangu kadri ikupendezavyo.**

Je, umempokea Yesu Kristo katika maisha yako? ______________________

Yesu yuko wapi hivi sasa kulingana na maisha yako?  Ufunuo wa Yohana

3:20 ___________________________________________________________

Unajua hivyo kwa mamlaka gani?  _________________________________

Soma 1 Yohana 5:10-13
Mpaji wa uzima wa milele ni nani? (aya11) _________________________

Uzima wa milele hupatikana wapi? (aya11) _________________________

Ni nani aliye na uzima wa milele? (aya 12) _________________________

Ni nani asiye na uzima wa milele (aya 12)  _________________________

____________________________________________________________

Kutokuamini ushuhuda wa Mungu juu ya mwanawe ni kusema Mungu ni

(aya 10) ____________    Je yeye ni? _____________

(Piga msitari maneno yasiyo sawa)
***"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili*** (tumaini kwamba, tuhisi kwamba, ubahatishe kwamba, ufanye kazi kwa ajili, mjue ya kuwa***) mna uzima wa milele."***  1Yohana 5:13)

Je, wajua ya kwamba wewe unao uzima wa milele? __________________

**PEKE YAKO**

Soma habari ya Nikodemu katika Yohana 3:1-8

Kariri vifungu vifuatavyo:

***"Na ushahidi wenyewe ndio huu: Mungu alitupatia uhai wa milele, na uhai huo uko kwa Bwana.  Yeyote aliye na Mwana wa Mungu anao uhai huo;asiye na Mwana wa Mungu, hana uhai."***  1 Yohana 5:11, 12

Je, ninawezaje kuyashinda mambo yale ambayo yangenifanya nisiishi katika maisha haya mapya?

Kipindi chetu kifuatacho ni  **"MAISHA MAPYA KATIKA USHINDI"**

Wakati __________ Mahali ____________________ Tarehe __________

# MISINGI YENYE NGUVU

Somo la Pili

**MAISHA MAPYA KATIKA USHINDI**

Rudia 1Yohana 5:11,12.______ Baada ya kukariri vyema hebu tazama katika Biblia kama umeisema sawa sawa.

Sasa umeanza maisha mapya katika Yesu Kristo, maisha yaliyo na nguvu nyingi unapoishi kadri Mungu alivyokusaidia. Lakini, kuna hatari ya kukata uhusiano wetu na Mungu tukitenda dhambi.

Katika kipindi hiki tutazungumza juu ya:
1. Dhambi ni nini.
2. Sababu zitufanyazo kutenda dhambi.
3. Kwamba Yesu Kristo ndiye suluhisho la dhambi.
4. Jinsi tunavyoweza kutumia suluhisho la Mungu kwa dhambi.

**1. DHAMBI NI NINI**

Dhambi ni kutenda yale nipendayo kinyume cha mapenzi ya Mungu. Dhambi ni hali ya kutokutii. Kama uwongo, udanganyifu, na kadhalika ni matokeo au tunda la kutotii.

Kabla ya kumpokea Kristo, dhambi ilikuzuia usiwe na uhusiano na Mungu. Soma Waefeso 2:1-5

Hali yako ya kiroho ilikuwaje? (aya 1) ______________________________

Ni nani aliyeongoza maisha yako? (aya 2) ____________________________

Ulikuwaje kiasili? (aya 3) __________________________________________

Sasa kwa kuwa umempokea Kristo, kwa rehema za Mungu, umefanyika kuwa nani? (aya 4, 5)

________________________________________________________________

Matokeo ya dhambi katika maisha yetu ni nini? Soma na ujadili aya hizi:

Warumi 6:23 — Warumi 2:8, 9

Yohana 8:34 — Zaburi 66:18

## 2. KWANINI TUNATENDA DHAMBI

Mungu ametupatia uhuru wa kuchagua kumtii yeye au kutokumtii. (Warumi 6:12,13). Kama wakristo, dhambi huzuia ushirika na Mungu. Inachukua muda kukua na kujifunza kufikiria jinsi Mungu anavyofikiria. Nia zetu zapaswa kuhuishwa. (Warumi 12:1, 2).

Majaribu na dhambi ni jambo la kawaida kwetu sote.
Sehemu tatu za majaribu ni gani?

1 Yohana 2:15, 16 _______________________________________________

____________________________________________________________

Je, majaribu ni dhambi? Waebrania 4:15 __________________________

____________________________________________________________

Tufanyeje ili majaribu yasituongoze kutenda dhambi?

1Wakorintho 10:13 _____________________________________________

____________________________________________________________

Mungu anatenda nini maishani mwako ili akupe njia ya kuepuka majaribu?

Wafilipi 2:13 ________________________________________________

____________________________________________________________

Soma Warumi 6:1, 2. Kama wakristo, ni kwanini tusiendelee kutenda dhambi?

____________________________________________________________

## 3. YESU KRISTO NDIYE SULUHISHO LA DHAMBI

Kusudi la kifo cha Kristo lilikuwa:

a. kuturudisha kwa Mungu
b. Kutulipia deni la dhambi zetu (1 Petro 3:18)

Soma maandiko yafuatayo:

> ***"Wakati mmoja nanyi mlikuwa mmekufa kwasababu ya makosa yenu na kwasababu nyinyi mlikuwa watu wa mataifa mengine. Lakini Mungu amewapa nyinyi uhai pamoja na Kristo. Mungu ametusamehe dhambi zetu zote; alifutilia mbali ile hati ya deni***

***iliyokuwa inatukabili na masharti yake, na kuifuta kabisa kwa kuipigilia msalabani."*** (Wakolosai 2:13, 14)

Kristo alizifia dhambi zako ngapi?

Wakolosai 2:13, 14 (angalia hapo juu) ______________________________

"Yote yamaanisha" yote - yaliyopita, ya sasa, na wakati ujao. Mradi sasa umempokea Kristo wewe umesamehewa kabisa. Kujua ya kuwa sasa umesamehewa dhambi kutageuzaje maisha yako?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**4. JINSI YA KUTUMIA SULUHISHO LA MUNGU KAMA ONDOLEO LA DHAMBI**

Kumbuka umesamehewa kabisa kwa kifo cha Yesu Kristo pale Msalabani kwa ajili yako, lakini, ili uendelee kuwa na ushirika na Mungu kila siku, sharti uziungame dhambi zote unazozijua.

Tunapoungama dhambi zetu, Kristo atafanya nini?

1Yohana 1:9 __________________________________________________

kuungama maana yake ni kukubaliana na Mungu juu ya dhambi yako.

(a) **Kubali** kwamba hiyo ni dhambi

(b) **Mshukuru Mungu** kwamba tayari ametoa msamaha.

(c) **Geuza** fikira zako mbaya (Toba)

(d) **Mruhusu Mungu** akuwezeshe kugeuza matendo yako.

(e) **Dai** msamaha wako hakika kwa imani na uishi maisha huru mbali na hatia.

Unapoungama dhambi zako na kudai msamaha wa Mungu utafurahia maisha ya ushindi dhidi ya dhambi.

**PEKE YAKO**

Kuwa na wakati peke yako na uandike orodha ya mambo yote maishani mwako yasiyompendeza Mungu. Kubali kwa Mungu kwamba hayo ni dhambi. Kwenye nakala yako andika I Yohana 1:9. Mshukuru Mungu kwamba amekusamehe dhambi hizi zote. Sasa ishi katika ushindi wa uhuru kama mtu aliyesamehewa. Rarua nakala yako kwa maana ni kati yako na Mungu.

Soma Zaburi 32
Daudi alishughulikiaje dhambi yake?

Alisikiaje moyoni kabla ya kukiri?

Alisikiaje moyoni mwake baada ya kukiri?

Soma Luka 15:11-32
Aya hizi zaonyesha mifano gani jinsi Mungu anavyotushuhulikia?

Kariri aya ifuatayo:

> ***"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."***
>
> 1Yohana 1:9

Ninawezaje kuwa na uwezo huu wa kuishi maisha haya mapya?

Kipindi chetu kifuatacho ni "**MAISHA MAPYA YENYE UWEZA".**

Wakati ________ Mahali ______________________ Tarehe ___________

# MISINGI YENYE NGUVU

Sehemu ya tatu

## MAISHA MAPYA YENYE UWEZA

Rudia 1Yohana 1:9 -Kariri kisha utazame Biblia kama umekariri sawa.

Maisha ya Mkristo ni maisha ya ajabu, ni makuu sana hakika hivi kwamba huwezi kuyaishi na ubinadamu. Bali tumepewa Roho Mtakatifu wa Mungu ili atuwezeshe kuishi maisha haya. Ni ajabu gani!

Katika somo hili tutajadiliana juu ya:

1. Uwezo wako mpya kama kiumbe kipya.
2. Chanzo kipya cha nguvu yako - Roho Mtakatifu
3. Jinsi ya kuongozwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu

### 1. UWEZO WAKO MPYA KAMA KIUMBE KIPYA

Soma 2 Wakorintho 5:17. Kama kiumbe kipya ni mambo gani yamepita?

________________________________________________

Nakili tabia na matendo fulani ambayo yamepita katika maisha yako.

________________________________________________

Umeona mabadiliko gani mapya katika maisha yako?

________________________________________________

Mabadiliko haya ni dhihirisho la ukweli kwamba wewe ni kiumbe kipya. (Umewekwa huru kutoka kwa nguvu za dhambi kwa maana asili yako ya kale ya dhambi imesulubiwa pamoja na Kristo.) Soma Warumi 6:6, 7

Ni kitu gani kilichosulubishwa? ____________________________

Lini? ____________________________________________

Kwa nini? __________________________________________

Soma Warumi 6:11-13. Tuyazingatieje maisha yetu sasa? (aya 11)

___________________________ na ______________________________

Funguo ya uhuru ni kukubali yale ambayo Kristo ametukamilishia juu ya msalaba kama ukweli. Sasa amua kuishi kama mtu aliye huru.

**2. CHANZO CHA UWEZA WAKO MPYA - ROHO MTAKATIFU**

Ulipompokea Kristo Kama Mwokozi wako, Roho Mtakatifu, aliye Mungu (I Wakorintho 2:11,12) alipiga muhuri uhusiano wako na Mungu (Waefeso 1:13) Naye atakuwa pamoja nawe milele (Yohana 14:16, 17)

**KWA NINI ROHO MTAKATIFU ALIKUJA?**

Soma kila aya kisha uunganishe maandiko ya Biblia uliyopewa na maneno yaliyoandikwa hapo.

| | |
|---|---|
| ____ Yohana 16:8 | a. Atuongoze katika kweli yote na atuonyeshe mambo yajayo. |
| ____ Yohana 16:13 | b. Kumletea Yesu utukufu |
| ____ Yohana 16:14 | c. Kutupatia Nguvu za kushuhudia |
| ____ Warumi 8:16 | d. Kuhukumu ulimwengu wa dhambi, haki na hukumu. |
| ____ Matendo 1:8 | e. Kutuhakikishia kwamba sisi ni watoto wake |

Shaidi ni nini? ________________________________________________

____________________________________________________________

Ni tunda gani (tabia au sifa) ambalo Roho Mtakatifu atazaa ndani yetu?

Wagalatia 5:22, 23 _____________________________________________

____________________________________________________________

Je, unatamani kuwa na sifa hizi katika maisha yako? __________________

Yakupasa ufanye nini? Yohana 15:4, 5 ____________________________

____________________________________________________________

**PIMA HALI YAKO YA KIROHO**

ASIYE KUWA MKRISTO - 1Wakorintho 2:14. Wote wasiotumaini kifo cha Yesu Kristo kama malipo ya dhambi zao.


MKRISTO WA KIMWILI - 1Wakorintho 3:1, 2. Wale wamtumainio Kristo kama mwokozi wao lakini sasa wanaishi kwa nguvu za mwili, wala si kwa nguvu za Roho.

MKRISTO WA KIROHO - 1Wakorintho 2:15. Wale wamtumainio Kristo kama mwokozi na wanamruhusu Roho Mtakatifu ili awape nguvu.

U - ubinafsi ukitawala
K - Kristo yuko nje ya maisha

U- ubinafsi ukitawala
K- Kristo yumo ndani ya maisha lakini ana puuzwa na haruhusiwi kuyaongoza maisha


K- Kristo yumo ndani ya maisha akitawala
U- ubinafsi unanyenyekea mapenzi ya Kristo naye Roho Mtakatifu anazaa tunda la Roho.




Mwongozo wa ubinafsi




Mwongozo wa ubinafsi




Mwongozo wa Kristo

Ni mviringo gani kati ya hii mitatu unaoeleza au kuonyesha maisha yako sasa hivi?

* Imenakiliwa kutoka kwa kitabu “Je, umefanya uvumbuzi wa ajabu wa maisha ya kiroho” kilicho andikwa na Dkt Bill Bright. Soma kijitabu hiki ili upate ufahamu zaidi.

**3. JINSI YA KUONGOZWA NA KUTIWA NGUVU NA ROHO MTAKATIFU.**

(a) Kiri dhambi yoyote unayoijua. (Zaburi 66:18)

(b) Toa kila sehemu ya maisha yako kwa Kristo. (Warumi 6:12, 13)

(c) Muombe Roho Mtakatifu akuongoze na akupe nguvu.

Twajua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu maana alituamuru tujazwe (tuongozwe na tutiwe nguvu).

***"Tena msilewe na mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho Mtakatifu."*** Waefeso 5:18

(d) Dai ahadi yake kwa imani.
Alisema angejibu kila ombi lililosawa na mapenzi yake.
Soma 1Yohana 5:14, 15
Je, ni mapenzi ya Mungu kwamba wewe uongozwe na Roho? ________

Unapo muuliza akuongoze, je, atafanya hivyo? ___________________

Unajuaje?__________________________________________________

Kuishi maisha ya kujawa na Roho ni kuishi maisha ya nguvu za Kristo kwa imani, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Ombi hili ni njia mojawapo ya kumuuliza Mungu kwa imani ili ayaongoze maisha yako.

**"Bwana Mungu, nimekutenda wewe dhambi kwa kuyaongoza maisha yangu mwenyewe. Asante kwa kunisamehe dhambi zangu. Sasa nakuomba uyaongoze maisha yangu. Kwa imani sasa ninadai nguvu za Roho Mtakatifu na mwongozo na ninakushukuru kwa kuniongoza."**

Je, umemwambia Roho Mtakatifu akupe nguvu? ______________________

Je, unaamini kwamba anayaongoza maisha yako sasa?__________________

Unajuaje? _____________________________________________________

**PEKE YAKO**

Juma hili ishi maisha ya imani yaliyotiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Chunguza nyakati ambazo wajiongoza mwenyewe, tumia alama ya tatu ya somo hili, na uendelee kudai mwongozo wake.

Kariri aya ifuatayo:

***"Mtu yeyote akiungana na Kristo huwa kiumbe kipya, mambo ya kale yamepita, hali mpya imefika."*** 2 Wakorintho 5:17

Je, twawezaje kuwa na usawa katika maisha yetu ya ukristo?

Kipindi chetu kifuatacho ni **"MAISHA MAPYA YENYE USAWA"**

Wakati_______ Mahali ____________________ Tarehe _____________


# MISINGI YENYE NGUVU

Somo la nne

**MAISHA MAPYA YENYE USAWA**

Rudia 2 Wakorintho 5:17_________ Soma katika Biblia baada ya kukariri moyoni mwako.

**KUWASILIANA**




Mawasiliano ni muhimu katika hali ya kukuza uhusiano wowote wenye maana. Kama wakristo tunaye Roho Mtakatifu atupaye nguvu za kuweza kuishi maisha ya usawa.

Katika kipindi hiki tutaanza kujifunza jinsi ya kuishi maisha ya usawa tunapo:

1. Mwabudu Mungu katika sifa na maombi.
2. Jifunza kwa Mungu kwa kusoma Biblia.
3. Shirikiana na kukua katika jamii ya Mungu.
4. Washuhudia watu wengine juu ya maisha yetu mapya.

**1. MUABUDU MUNGU KATIKA SIFA NA MAOMBI**

Kumuabudu Mungu ni kumtambua yeye kuwa ni muhimu kupita mtu yeyote yule au kitu chochote kile maishani kwani yeye pekee ndiye mstahili.

**SIFA**

Mungu hupendezwa na sifa za watu wake.
Soma Zaburi 33:1-3 Aya hizi zasemaje kuhusu sifa?

_____________________________________________________________

Dunia yote yatangaza ukuu wa Mungu. Kwa nini basi umsifu?

Waefeso 1:3 _________________________________________________

**MAOMBI**

Ni vitu gani tunavyopaswa kumuomba Mungu atupe?

Wafilipi 4:6 ________________________________________________

Kwa nini ni muhimu kutoa shukurani? ____________________________

Mungu hataki sisi tufadhaike juu ya kitu chochote. Mapenzi yake kwetu ni

gani? Wafilipi 4:7____________________________________________

Kusudi la maombi katika Yohana 16:24 ni nini? ______________________

_____________________________________________________________

Mungu anakupenda - wewe ni mtoto wake. Anataka wewe uje kwake kwa jambo lolote linalokuhusu. Je, unajambo lolote sasa hivi ambalo twaweza kuliombea pamoja?

Hebu tutulie na tuombe kwa ajili ya mambo yanayotuhusu. Tuanze kwa kumsifu kwa jinsi yeye alivyo.

## 2. JIFUNZE KWA MUNGU KWA MAFUNDISHO YA BIBLIA

Kama baba mpenzi yeyote, Mungu anataka sisi tujifunze kutoka kwake. Njia zake ni kuu kushinda zetu, ya kwamba hatuwezi kamwe kuyaelewa mawazo yake. Inagharimu wakati na juhudi.

Soma Warumi 12:2

Yatupasa tusiwe namna gani? ____________________________________

Yatupasa tuweje? ____________________________________________

Namna gani? _______________________________________________

Matokeo yatakuwaje? _________________________________________

_____________________________________________________________

Je, hiyo ni tamanio yako? _____________________________

Neno la Mungu, yaani Biblia ndilo maagizo yake kwetu sisi ilituweze kuhuishwa nia zetu na tufikirie ukweli wa Mungu.

Soma 2 Timotheo 3:16,17. Eleza faida nne zinazopatikana kwenye mafundisho ya Biblia.

1. ____________________________ 2. ______________________________

3. ____________________________ 4. ______________________________

Itakubidi usome na kujifunza Biblia mara kwa mara kwa muda mwingi. Anza leo na usome sura moja kutoka injili ya Marko kila siku.

**3. UWE NA USHIRIKA ILI UKUE KATIKA JAMII YA MUNGU**

Mungu anataka sisi tufurahie ushirika wa wakristo wengine kama sehemu ya jamii yake.

Waebrania 10:24, 25 yasema kwamba haitupasi _________________________

_________________________________________________________________

Utafaidikaje kwa kushirikiana na wakristo wengine? ____________________

_________________________________________________________________

Kama huna ushirika anza kwenda kwa kanisa linaloamini Biblia na Kundi la Uzima (ama ushirika mdogo). Hii itakupatia moyo.

KUKUA PAMOJA

Chukua hatua nyengine ya kukua katika ufahamu wa Neno la Mungu. Amua kuhudhuria ukufunzi Wenye Nguvu wa Mmoja-kwa-Mmoja juma lijalo. Kunaye mtu atakayekutana nawe.

Kwa nini tuwe na bidii? II Timotheo 2:15. Andika aya hii:

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

## 4. SHUHUDIA MAISHA YAKO MAPYA KWA WATU WENGINE

Sasa umeanza kuyaelewa mazuri yaliyo yako kwasababu ya maisha yako mapya katika Kristo. Kufikia sasa umeona mabadiliko gani?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

Je, ni mabadiliko ambayo jamii yako na rafiki zako wangefurahia? _____

Kando ya kuwa wanaweza kuhisi furaha ya kumjua Kristo kibinafsi, kwa nini yakupasa kuendelea kushirikiana nao?

Matendo ya Mitume 4:12 ________________________________________

Je, twaokolewa kutokana na nini? ________________________________

Unapomfuata Kristo, yeye atakufanyia nini?

Marko 1:17 __________________________________________________

Ni nani ambaye ungependa kumkaribisha kwenye Kundi letu la Uzima au shughuli yoyote ya kanisa ili waweze kuanza kuusikia ukweli wa Mungu?

_______________________________________________________________

______________________ Utawakaribisha lini? ______________________

Ungelipenda mimi nikusaidie? ___________________________________

Ongea kuhusu Ukufunzi Wenye Nguvu wa Mmoja-kwa-Mmoja.
(Soma katika maandishi ya Ukufunzi Wenye Nguvu.)

Kariri kwa moyo aya ifuatayo:

> ***"Jitahidi kupata kibali mbele ya Mungu kama mfanya kazi ambaye hufundisha sawa ule ujumbe wa kweli."***
>
> 2 Timotheo 2:15

Hakikisha unaendelea kushuhudia mtu Mmoja-kwa-Mmoja katika Ukufunzi Wenye Nguvu.

# UKUFUNZI WENYE NGUVU

**Mmoja-kwa-Mmoja**

**NAFASI NZURI**

Wakristo wengi siku hizi wangependa kuwa na nguvu, uwezo na maisha yakutosheleza kama ilivyoandikwa katika waraka wa Agano Jipya. Haikuwa michezo kwao, bali uvamizi wa maisha yao na maisha mapya waliyoyaita "Kristo anaishi ndani yao."

Kupata maisha haya mapya kunahusiana na mwito wetu kwa Neno la Mungu. Katika mfano wa mpanzi, Yesu anaonyesha kwamba watu huitikia Neno lake katika njia nne. Soma Mathayo 13:3-9 na 18-23.

Ni udongo gani ungelipenda usimamie maisha yako?

Ukufunzi Wenye Nguvu ni nafasi nzuri itakayokusaidia kujenga mwenendo stadi katika Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na kujifunza jinsi ya kufundisha wengine.

**UKUFUNZI WENYE NGUVU NI NINI?**

1. Ni mfululizo wa mafundisho yaliyonukuliwa kukusaidia wewe uzidi kumpenda Mungu na watu wengine.

2. Una vipindi tisa vya mafundisho ya Mmoja-kwa-Mmoja ambayo hutumiwa na mtu mmoja kumfundisha mwengine ambaye naye atamfundisha mtu mwengine.

3. Tutakutana mara moja kwa wiki kwa mafundisho ya Ukufunzi Wenye Nguvu wa Mmoja-kwa-Mmoja kwa muda wa saa moja au saa moja unusu. Tutashiriki na kuomba pamoja na kujifunza kanuni za Biblia.

**KWA NINI MMOJA-KWA-MMOJA?**

1. Ukufunzi wa muda mchache wa Mmoja-kwa-Mmoja huongezeka kwa haraka sana. (Njia nzuri zaidi yakumfundisha mwengine).

2. Karibu kila mmoja anaweza kumfundisha mtu mwengine. Mwanamume humfundisha mwanamume mwengine na mwanamke humfundisha mwanamke mwenzake.

3. Ni ubora zaidi ya kwamba wewe uinuke kuwa kiongozi.

4. Unakuwa mtu wa kudiriki.

5. Inakusaidia wewe uwe mtiifu zaidi kwa Kristo unapofanya ukufunzi shupavu.

6. Utakuwa na nafasi ya kujenga uhusiano wa Kristo wenye nguvu.

7. Hutupa nafasi nzuri ya kupanga nyakati zetu za Ukufunzi Wenye Nguvu pamoja.

**LENGO LA UKUFUNZI WENYE NGUVU NI:**

1. Kukusaidia ukue katika uhusiano wako na Mungu na upate nguvu Zake. (Waefeso 3:16, 17)

2. Kukusaidia upate ufahamu zaidi wa Neno la Mungu na kukutia nguvu katika maisha yako ya maombi. (Zaburi 1:2, 3; Wakolosai 4:2)

3. Kukusaidia kuwa na ushirika wa Kristo wenye nguvu na watu wengine. (1Wathesalonike 3:12)

4. Kukusaidia kujibu maswali yako yanayohusu maisha ya Mkristo. (Matendo ya Mitume 17:11)

5. Kukusaidia kupata msingi bora wa maisha yako na kukufundisha jinsi ya kuwasilisha kwa mwengine. (II Wakorintho 5:18).

**NIFANYEJE ILI NIWEZE KUHUSIKA KATIKA UKUFUNZI WENYE NGUVU?**

1. Tamani kukua katika uhusiano wako na Kristo.

2. Uwe mtu wa kufundishika - uwe tayari kujifunza na kuchangamana na watu wengine.

3. Uwe tayari kuhudhuria mafundisho ya kila juma na ununue kitabu cha mafundisho.

4. Uwe tayari kufanya kazi zote upewazo.

**JE, UNAWEZA KUOMBA ILI UHUSIKE?**

Nitakuita tarehe ___________________ kwa jibu lako.

# MISINGI YENYE NGUVU

## TARATIBU YA VIONGOZI

Unayo nafasi ya manufaa ya kusaidia kuimarisha Mkristo mchanga katika imani na mwenendo wake ndani ya Kristo Yesu. Wanapoanza "maisha mapya", utakuwa na furaha ya kuwaona wakikua na kukomaa ili wawe wanafunzi dhahiri wa Yesu Kristo. Hii ni huduma moja wapo muhimu unayoweza kuipata kwa maana iko katika kiini cha mwito mkuu. Katika Mathayo 28:18-20 yasema kwamba yatupasa ***"kuenda na kufanya wanafunzi".*** Yaendelea kusema jinsi tunavyoweza kufanya wanafunzi – ***"kwa kuwafundisha kuyatii yote niliyokuamuru."*** Kristo mwenyewe ameamrisha huduma yako na ameahidi kukupa nguvu siku zote. Mtume Paulo asema katika Wakolosai 1:28, 29.

> ***"Kwa sababu hiyo tunamhubiri Kristo kwa watu wote; tunawaonya na kuwafundisha wote kwa hekima yote, ili tuweze kumleta kila mmoja mbele ya Mungu akiwa amekomaa katika kuungana na Kristo. Kwa madhumuni hayo mimi nafanya kazi na kujitahidi nikiitumia nguvu kuu ya Kristo ifanyayo kazi ndani yangu."***

Jukumu letu ni kuwa na bidii katika kuwafundisha wanafunzi wetu. Jukumu la Mungu ni kutupa nguvu na kumkuza yule mwanafunzi. Mungu atatutumia sisi tunapokuwa waaminifu kutimiza jukumu letu.

## LENGO LA UFUATILIAJI BORA

Utakuwa wa msaada zaidi kwa Mkristo huyu mchanga kama unaelewa ni jambo gani unalotaka kutimiza.

**Lengo la vipindi hivi vinne ni:**

1. Kumsaidia mtu yule aelewe misingi ya ukweli ambayo Neno la Mungu latufundisha tuishi kwalo.

2. Kumsaidia mtu yule aweke imani yake katika Neno la Mungu na ajifunze kuishi katika kanuni za Mungu.

3. Kumsaidia mtu yule aanze kufanya urafiki na wewe pamoja na wakristo wengine.

4. Kumkweza mtu yule akomae na awe na ibada timilifu kwa Mungu.

## KUANDAA MKUTANO WAkO WA KWANZA

Kama ungelikuwa na nafasi ya kushuhudia injili na kuwasaidia wawe na imani ya binafsi katika Yesu Kristo akiwa mwokozi wao, au kama umepewa jina la mtu umfuatilie, shuhudia jinsi mtu mwengine alivyokusaidia wewe kukua kama mkristo mchanga. Wasaidie kukua. Yakupasa kusema, "**Nina furaha sana ya kuwa umefanya uamuzi huu. Ni muhimu sasa ujifunze kuyafurahia maisha yako mapya yote. Tafadhali tukutane pamoja siku chache zijazo tuangalie ukweli fulani utakaokusaidia kuishi maisha mapya katika Kristo?"**

Wanapokubali, waambie siku gani mtayokutana, saa na mahali pa mkutano. Kama hawatapatikana (kwa ajili ya mfuatizio wakati huu), jaribu kuwakaribisha kwenye ushirika wenu au shughuli zozote za kanisani.
Peleka uamuzi wa mtu huyu kwa yule aliyekupa jina lake.
Uwe rafiki. Waombee daima.

## KUJENGA UHUSIANO MWEMA

Jambo muhimu katika ufuatiliaji bora ni ule uhusiano unaoujenga. Kama rafiki mwema:

1. Mpende mwanafunzi wako:

    - Sema jina lake mara kwa mara, mtazame na utabasamu.

    - Muulize kuhusu maisha yake na mambo apendayo.

    - Sikiliza. Mwitikie kwa furaha anapozungumza.

    - Gundua yote yanayo muhusu.

    - Uwe tayari kumtimizia mahitaji yake ukiweza.

    - Muonyeshe jinsi Yesu alivyo muhimu katika maisha yake.

    - Mkubali kwa upendo, sio kwa matendo.

    - Muonyeshe msisimko na shauku kwa ukweli mpya anaougundua.

    - Usionyeshe kutoridhika na maswali au majibu yake.

    - Ongea wema kuhusu watu wengine.

2. Muelezee mwanafunzi wako juu ya maisha yako:

- Elezea jinsi Yesu alivyokufaa maishani mwako.
- Uwe mfano mwema kwa mambo yote.
- Uwe dhahiri katika mahitaji yako mwenyewe.
- Uwe wazi kushiriki jinsi unavyotenda Neno la Mungu.
- Sema hujui kama huwezi kujibu swali fulani. Kwa pamoja mjaribu kupata jawabu.
- Onyesha ujasiri wako katika Mungu.
- Uwe na msisimko.
- Uwe rafiki - muwe na wakati pamoja mbali na wakati wa ufuatizo. Fanyeni mambo ambayo nyote wawili mwayafurahia.
- Muombee mwanafunzi wako kila mara.

**VIPINDI VYA UFUATIZIO**

Kabla ya kukutana pamoja, kuwa na ufahamu kadri wa kila kipindi. Kwa ufuatizio bora, fuata maoni haya rahisi:

1. Chagua mahali pa kukutania palipo pazuri na pasipo na usumbufu.

2 Amkuaneni. Mara ya kwanza mnapokutana, iweni na wakati wa kujuana na kujuana hali. Uliza kuhusu jamii, kazi, nk. Kila juma chukua wakati wa kuwaonyesha kwamba unahusika na maisha yao. Hakikisha kuacha dakika 30 za kurudia mafundisho..

3. Geukia kipindi cha kwanza kwa kusema, "**Ninafuraha kwamba tumeweza kukutana pamoja na kujuana. Kama Mkristo mchanga, utayafurahia mambo yote tutakayojifundisha. Vipindi hivi vitatusaidia kuzungumza juu ya mambo yenye maana."** Kwa vipindi vifuatavyo mwambie "**juma hili tuta soma (soma kichwa cha mafundisho)."** Onyesha kuridhishwa na umuhimu wa kila kipindi.

4. Kila juma lete kipindi chako ulichokamilisha pamoja na kipindi kipya cha mwanafunzi wako.

5. Jadili kila sehemu ya somo.

a. Mbadilishane mnaposoma somo lile na aya za Biblia. Mistari iliyo katikati ya aya na isomwe tu wakati kuna swali juu ya jambo lisemwalo.

b. Huenda ukahitajika kusoma Biblia yako na mwanafunzi wako katika kipindi cha kwanza lakini mhimize kubeba Biblia yake kwenye kila kipindi. Kama hana Biblia msaidie ili apate kuwa na moja. Msaidie mwanafunzi wako afahamu vitabu vya Biblia. Muonyeshe yaliyomo katika Biblia kisha umueleze jinsi Biblia imegawanywa katika vitabu, sura, aya, milango au vifungu. Kuwa mvumilivu, mwachie nafasi peke yake aweze kutafuta na kutambua vifungu.

c. Changamsha majadiliano kwa kuuliza maswali zaidi kama:

- Ni kitu gani zaidi unachokiona katika aya hii?
- Wafikiria Yesu alimaanisha nini aliposema ________________?
- Kwa maneno yako mwenyewe, ungelisemaje hii?
- Je, hii yakuhusuje leo?
- Je, umejifunza chochote kuhusu maisha yako katika kipindi hiki?

**PEKE YAKO**

Mhimize mwanafunzi wako kukamilisha kazi zile ndogo nyumbani ili apate nguvu za kutimiza kanuni za Biblia zinazofundishwa katika kila kipindi.

**AYA YA KUKARIRI**

Sisitiza umuhimu wa kuwa na Neno la Mungu mioyoni mwao. Waambie ya kwamba kwenye kipindi kinachokuja watasema andiko hili bila kusoma katika Biblia.

**FUNGA**

Panga wakati wa kukutana tena.

Mpe mwanafunzi wako "Cheti cha Kuhitimu" anapokamilisha kipindi cha nne. Iwezekanapo, mkabidhi cheti chake katika ushirika wenu.

Funga kwa maombi.

Katika mwisho wa kipindi cha 4 wahimize waendelee na Ukufunzi Wenye Nguvu.

# Cheti cha Kuhitimu

**Hii ni kuthibitisha kwamba**

________________________________

**Amefaulu kumaliza mafundisho ya**

***Misingi Yenye Nguvu***

____________________

**Tarehe**

____________________

**Mwalimu**